# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

Mwaka XXII – N. 3, March 2020

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


Mhariri

## Mzeituni unaoongelewa kwa ajili ya safari

Kwa kumalizia adhimisho la miaka185° ya maisha ya Waabuduo Ulimwenguni, tarehe10 february huko Acuto, katika bustani ya nyumba Mama, ulipandwa mti wa mzeituni. Waabuduo waliokuja kutoka sehemu mbali mbali za Ulimwengu hapa Roma kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Wakubwa wetu wa mwaka 2020, ambao walichukua nafasi ya tukio. Mara yalifuata maandamano kuelekea katika kikanisa Kidogo cha Acuto cha nyumba Mama; ambapo mbele ya Altare ya Mtakatifu Maria De Mattias kila Sista alibeba kiasi cha udongo wa ardhi alikotoka huku Mkuu Wa Shirika akiwa amebeba mti wa Mzeituni. Kulikuwa na hali ya manyunyu ambayo ilitufanya tusitoke nje. Huku tukiimba na kusifu Damu ya Yesu, tuliandamana kuelekea mahali palipoandaliwa kwa ajili ya kuupanda mti huo. Katika Sala ya shukrani na Baraka ambayo ilitolewa na Sr. Nadia, kila Mkuu na mwakilishi aliweza kuweka udongo katika mizizi ya mti ule mchanga. Katika maajabu ya kuangalia aina ya rangi na vitu ambavyo dunia iliwasilisha, tulijiuliza kama kweli ule mti utastawi! Baada ya muda wa wiki moja mtunza bustani alituambia kwamba mti ulikuwa unaendelea vizuri.

Ndivyo ilivyo kwa kitu chochote kinachoanza unahitajika ujasiri wa kukabiliana na hatari, ni dhahiri kwamba mzeituni ulipopandwa ulikuwa katika hatari ya kutositawi na kutoa maua kwani ulikuwa umehamishiwa kwenye udongo tofauti. Ni hatari isiyoweza kuepukika kwa sababu anayejihatarisha anaweza kuzaa na kutoa maua. Rangi za aina tofauti za udongo na vifaa tofauti havizuii mmea kuchukua mizizi, maua, lakini kwa utofauti wao huvipa lishe zaidi na kwa hivyo hufanya kuwa na nguvu, katika kuchanua maua, ila katika tofauti zao hutoa zaidi uhai na kujilisha na kuwa na nguvu zaidi. Inahusiana zaidi na mazungumzo ya Waabuduo ambayo baada ya miaka 185 ya kihistoria wanataka kuonyesha. Wito wa kupokea njia za mageuzi maana yake ni kupoteza kile ambacho kinafahamika daima, ambacho daima kimeaminika na kufanyika daima; inabidi kukiacha kile ambacho hakileti uhai, siyo tu swala la kuwa huru ila kujaribu kutoa nafasi ya kitu kipya ambacho kipo ndani ya kila mmoja wetu. Kufanya nafasi kwa Roho anayetuita na kutufanya wapya kwa kupyaisha ukweli unaotuzunguka, "kufufua" Karama.

***Sr Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Muhtasari


*Muhariri*
- Mzeituni unaoongelewa kwa ajili ya safari 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Mkutano wa Tume ya Ratio Formationis 2

*Kwa namna ya pekee Albania*
- Utume uliowekewa alama ya Msalaba 3

*Toka Ulimwengu wa ASC*
- Utakatifu wa Stanley Rother huko Wichita 5
- Mabadiliko na mageuzi 5
- Kama ingekuwa 6
- Kumbu kumbu ya… 6
- Mkate na Mauaridi 7
- Habari kutoka Australia 8

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- Sala dhidi ya usafirishaji haramu 9

*Katika Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 10
- Sherehe za Nadhiri za kitawa 10
- Siku za kuzaliwa: tusherehekee Uhai 10
- Waliorudi nyumbani kwa Baba 10

# Mkutano wa Tume ya Malezi

Ili kutupa Uhai, Baba anatuita kuwa kama Mwanaye Yesu, kujisanidi kwake, na kuhisi usikivu wake. Maria De Mattias amejibu wito huu wa kumfuata Yesu Msulibiwa na Mfufuka mpaka mwisho.

Kwa hisia hizi, Mkuu wa Shirika, Sr Nadia Coppa, na Kamati yake, wamesikia umuhimu wa kufikiria juu ya kichwa hiki cha Malezi. Kisha waliunda Tume kwa ajili ya huduma hii, iliyoundwa na: Sr. Danijela Anić, ASC – Region ya Zagabria, Sr. Beth Simone Almeida Andrade, ASC – Region ya Brasile, Sr. Orsolina Griffini, ASC – Region ya Italia. Sr Wiesława Pzybylo – wa Kamati Kuu ambaye aliteuliwa kama Mratibu wa kikundi cha kazi. Mkutano wa kwanza ulifanyika tarehe 8 January c.a. kwa njia ya Skype akiwepo pia Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika. ambaye alielezea madhumuni ya kazi kwa tume.



Kuanzia tarehe 29 January mpaka tarehe 1 February c.a. tume ilikutana Roma kwenye Nyumba Kuu. Uwepo wa Sr. Nadia kwetu ulikuwa ni sababu ya furaha hasa zaidi kututia moyo kutia ladha na mwanga kwa huduma hii muhimu kwa Shirika.

Zilikuwa ni siku za kufahamiana na kuheshimiana, ya kubadilishana uzoefu, ya ufafanuzi juu ya miongozo ya mikutano itakayofanyika baadaye.

Tunamshukuru Padre Leonello Leidi, CP, Mtaalamu wa Sheria ya Kanisa, ambaye ataisindikiza Bodi kwa marekebisho ya sheria inayofaa. Pia shukrani nyingine zimwendee Prof. Méthode Gahungu

Ambaye alijitoa kwa umakini na kutuelewesha juu ya Malezi. Alituonyesha njia ya kwenda kuendeleza mpango wetu wa mafunzo na akatutia moyo kila mtu ajue uzuri wa kumfuata Kristo.

Ukijua mwelekeo wa kusonga mbele, maisha yana maana, hata kama si wote wenye majibu na moyo wenye Upendo na bidii ya kwenda kuutafuta Ufalme wa Mungu.

Kwa imani tuuombe Utatu Mtakatifu utusindikize katika safari hii na kutupatia neema ya kukaribisha hekima ya watu wetu katika roho ya umoja wa kimataifa na ya kiutamaduni.

Maria De Mattias atuwezeshe kujibu changamoto za nyakati zetu kwa kufuata mpango wetu wa malezi pamoja na taratibu zinazoangazwa na Karama ya Shirika letu.

***Sr. Beth Simone Almeida Andrade, ASC***

# Utume uliowekewa alama ya Msalaba

*Aya juu ya Waabudu wa Albania katika historia ya Shirika imeandikwa na Sr Antonietta Maraone. Ufuatao ni muhtasari wa historia yao.*





Hebu tuangalie kidogo kumbukumbu yao, Waabuduo walifika Albania tangu Mwezi wa Tisa mwaka 1939. Walialikwa na Mapadre wa Coventuali wa Lishnia, Mji uliopo kati ya Durazzo na Valona, ambapo wangekuwa na uwanja mkubwa wa utume.

Waabuduo wanne wa kwanza: Sr. Palmina Canalicchio, Pia Garelli, Elena Boco e Giuditta Curati, walioalikwa na Sr. Agnese Maroncelli aliyekuwa provinci ya Cagli, licha ya ugumu wa lugha, umaskini wa vitu, kwa sababu ya ugumu wa maisha ambao ni sadaka kubwa, walitafuta kujibu mahitaji ya kimwili na ya kiroho ya watu katika miaka ile ya 1941 walipofungua chekechea na maabara na walikuwa wakitibu wagonjwa. Ulikuwa ni wakati wa wakomunisti na familia zilikatazwa kuwapeleka wasichana shuleni, huduma za upasuaji wa wagonjwa hazikuruhusiwa, vile vile kulikuwa na tishio la moto. Mateso ya Kanisa na kidini na Wakomunisti yalizidi kuongezeka hadi watawa, pamoja na wamishonari wengine, walifukuzwa na kulazimishwa kurudi makwao; 86 walifika Brindisi mnamo Machi 12, 1946.

Kwa Waabuduo kuweza kurudi Albania walilazimika kungoja hadi miaka ya tisini ambapo ukuta wa Berlin ulianguka. Ilikuwa Caritas ya Apulian na mkurugenzi wake Sr Maria Bambina Centra, Mwabudu wa Damu ya Kristo, pia kuupatia mkoa wa Bari fursa ya kurudi na kutoa huduma kwa watu walioharibiwa kiutu na kithamani, kwa sababu ya miaka hamsini ya udikteta wa kikomunisti.

Jumuiya ya Durazzo na Mamurras, ilifunguliwa mara moja baadaye. Shukrani kwa ushuhuda wa Waabudu wa Italia ambao walifuatana na wale ambao bado wanafanya kazi huko; kwa namna ya pekee Jumuiya ya Waabuduo wa Albania na shukrani kwa ushuhuda wa maisha na roho ya kitume ya Sr Agnese Bianchi, ambao wametoa matunda ya miito, ASC wanne wa Albania, leo katika huduma ya Kanisa mahalia, kuweza kuponya majeraha ya watu wao ili kurejesha matumaini.

Katika muktadha huu wa wizara, pamoja na watu na miongoni mwa watu, usiku wa Novemba 26, 2019 tetemeko la ardhi lenye nguvu lilitikisa safu hii ya ardhi iliyozunguka Bahari ya Adriatic, kwa mara nyingine ikileta mateso na vifo.

Mkuu wa Shirika, Sr Nadia Coppa, aliwaalika wanashirika kuonyesha alama ya mshikamano kwa faida ya watu walioathiriwa na msiba huu.

Jioni ya tarehe 25 Disemba, siku ya Noeli, Sr. Nadia, siku chache baada ya kurudi kutoka Tanzania kwa ajili ya kazi ya Utume, aliendа kuwatembelea Masista, na huko akakuta ulikuwa ni msimu wa baridi na hali ilikuwa ngumu; lakini watu waliupokea kwa furaha ya kindugu uwepo wake.

Masista, Sr. Suela Pepa, Sr. Anna De Robertis, huko Durazzo na Sr. Natalina Hoti pamoja na Sr. Anna Carcagnì huko Mamurras, walifanya kazi ya kuzisaidia familia ambazo zilikuwa hazina makazi Anashukuru kwa ukarimu wa wanashirika kwa ujumla. Wanapeana fursa ya kununua vyombo, Container ambalo litatumika badala ya nyumba kwa ajili ya familia zilizoachwa bila makazi.

Masista wanaendelea kutoa mahitaji ya kimwili na kiroho kwa wale ambao bado wanahitaji.

Sr. Suela Pepa, animatrice wa costellazione Durazzo Mamurras aliyetuandikia barua hii….

*Wapendwa Masista ASC,*

*kama mnavyojua Albania ilikumbwa na tetemeko kali la ardhi mnamo Novemba 26, 2019, ambalo lilichukua uhai wa watu wengi, hisia, lakini pia nyumba na hali ya siku zijazo. Zaidi ya mwezi na nusu umepita na jiji la Durres, Tirana, Laç na maeneo ya pembeni bado hayajaamuliwa kama yatakuwa makazi ya watu au la. Na nyumba za watu wengi lazima zibomolewe au kujengwa tena, wakati huko Thumana kuna ukiwa mkubwa, huko kuna ujenzi lakini haijajulikana bado, vipi, wapi na nani.*

*Tunamshukuru Mungu ingawa mshtuko unaendelea lakini ni kwa nadra na ni kidogo zaidi na, kwa vile hauathiri, lakini uharibifu uliobaki unaendelea kuwapo, hata kama serikali imeondoa mara moja kifusi cha majengo yaliyoanguka. Katika baadhi ya vitongoji, kama vile ile ambayo jamii iko katika Durres, ambapo inaonekana hakuna uharibifu mwingi nje, nyumba ndani zote zina nyufa kubwa na majeraha, maisha yanaonekana kuwa yamekoma. Ukimya wa mchana na giza la usiku hushuhudia hili.*

*Watu ambao walikuwa wamepanga katika hoteli wanaambiwa kwamba wanapaswa kuondoka kwa sababu hawawezi kukaa huko tena, msimu wa watalii unakaribia na hoteli zinapaswa kuwa tayari.*

*Watu wengi hukaribishwa na jamaa kulala usiku, mara nyingi na magodoro sakafuni kutokana na nafasi kuwa ndogo na wengine wengi wanakaa nyuma ya nyumba zao wenyewe katika hema wakati wa majira ya joto au kujitengenezea wenyewe na plastiki.*

*Kama mnavyoweza kuelewa vizuri na kufikiria, katika siku hizi kumekuwa na upepo mkali sana, ambao kwa nyakati zingine umepasua mapazia, hali za watu hawa ni za kusikitisha kweli. Ni hali ngumu kwa watu wazima na tunafikiria kwa watoto, ambao wanajaribu kujihifadhi kwa mablanketi huku anga likiwa wazi.*

*Kama katika familia halisi, iliyounganishwa siyo kwa Damu ya mwanadamu, bali kwa Damu ya Kristo, mmetufanya tuhisi mapendo yenu na umoja wenu, siyo tu kwa njia ya Sala bali kwa njia ya simu, na barua pepe.*

*Tunataka kuwashukuru kila mmoja wenu, kama mtu binafsi na kama Jumuiya, ambapo kwa ukarimu mkubwa na kazi ambayo mmeifanya kwa ajili ya kukusanya kiasi cha 10.000€ ambacho ni kwa ajili ya Utume wetu zilizoletwa na sr Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika, ambaye alikuja kututembelea na kugusa kwa mkono ukweli wetu wa siku hizi. Kwa kweli tulishukuru sana na tulijisikia kwamba hatuko peke yetu.*

*kwamba kwa niaba ya utume wenu, ambao ulikuja kwetu kupitia Sr Nadia Coppa, Mkuu waandamizi, aliyekuja kututembelea na kugusa ukweli wetu siku hizi. Tunakushukuru sana kwa sababu hatukujisikia peke yetu.*

*Thumana Tumetumia mchango wenu kununua moduli za makazi kwa familia katika kijiji cha Tuman, kwa wale ambao tuliona kwamba walikuwa na "nyumba ya kukaa, katika siku hizi huzuni kwao na haswa kwa watoto, walilia na hawakujua tena jinsi ya kushukuru kutoa kile walichokuwa nacho, karanga chache, chupa ya kinywaji kwa ajili ya kuyeyusha chakula / grappa, jozi ya soksi za pamba ... na asante bila mwisho .. Hawakosi kumwombea na kumbariki kila mwabudu. kutoka kwa familia zilizopokea moduli za makazi. Sisi ASC ambao tunafanya kazi hapa tunayo furaha kubwa kuona tabasamu tena kwenye nyuso za watoto na za watu wazima.*

*Ukweli ni kwamba mahitaji ni mengi, lakini tunajaribu kujibu kilio cha wale ambao wamekata tamaa na wasio na tumaini na tunafanya kile tunachoweza pamoja na wale wanaotusaidia.*

*Kwa niaba ya Jumuiya ya ASC wa Albania na kwa niaba ya watu waliosaidiwa tunataka kuwashukuru kwa ukarimu wenu na kumwomba Bwana awafanye muwe wanawake wenye ukarimu ambao wanaweza kufungua mioyo yao kwa kilio cha maskini, kwa walio wa mwisho na wale ambao wamesahauliwa na wote.*

***Sr. Suela Pepa, ASC***

Eneo la Bara: Amerika
Region ya USA

## Utakatifu wa Stanley Rother huko Wichita

Padre Stanley alikuwa ni Padre Muamerika ambaye alikuwa akitoa huduma yake ya kimisionari huko Guatemala wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Amerika ya Kati. Aliuawa na wanaume watatu ambao waliingia nyumbani kwake asubuhi na mapema tarehe 28 Julay 1981

Sababu yake ya kuweza kutangazwa Mtakatifu ilianza mwaka 2007, na 2016, Papa Francesco alimtambua rasmi kuwa Shahidi wa Imani. Alitangazwa Mwenye Heri Mwaka 2017.

Kwenye picha Sr. Marita Rother, ASC, Dada yake, alijionyesha wakati tulipotembelea Kikanisa hiki kipya cha Mwenye Heri Padre Stanley Rother, tulikutana nje ya Kikanisa kipya cha Bikira Maria mama wa Agano Jipya katika kituo cha ASC cha Wichita.

Marita alitoa masalia ya kwanza (mabaki ya mwili) na sanamu ya Padre Stan. Msimamizi wa Kituo cha Wichita, Greg Lohkamp aliweka ulinzi wa masalio hayo.

Utakatifu wa Padre huyu unatutia moyo wa kuendelea na mapambano ya kila siku na kumpa Mungu wetu kila kitu.



**_Sr. Fran Schumer, ASC_**

## Mabadiliko na Mageuzi

Kauli mbiu ya maelekezo ya Mkutano Mkuu wa 2017 inatualika kukubaliana na mchakato wa mabadiliko.

Tangu tulipopata mwito huu, nimeisikiliza podcast, nikisoma na kutafakari juu ya mada hii.

Hii ilisababisha nia mpya katika Enneagram, tathmini ya utu wa tabia ya kwanza ambayo nilikutana nayo miaka kama 40 iliyopita.

Nimegundua kuwa leo imeleta kuzaliwa tena kati ya vizazi vichache.

Mojawapo ya mambo ambayo ninayathamini juu ya Enneagram ni kwamba ni mwaliko wa kugundua wewe ni nani, kwa kutegemea motisha ya mawazo na vitendo vyako.

Imeibuka kwa miaka kujumuisha zana za ukuaji wa afya na uadilifu. Kusudi ni kuwa mtu ambaye Mungu alikuumba. Hiki ndicho ninachokiita mchakato wa mabadiliko.

Suzanne amepangilia, katika podcast yake "The Enneagram safari", hufanya tofauti hii kati ya "mabadiliko" na "mabadiliko".

Anaendelea kusema, "Njia yetu ya kufahamiana ni nzuri kiasi kwamba inatuwezesha kuona tofauti zetu. Wakati sisi "tunabadilika", tunaongeza vitu kwa utu ambao ni wa hali ya juu. Tunapaswa kujiangalia kwa njia isiyo ya kuhukumu na kuondokana na kile ambacho hakitusaidii sisi na wengine.

Nimefikiria juu ya tofauti ambayo Suzanne hufanya kati ya mabadiliko na mabadiliko, na nimeona ushahidi wa hili katika mazungumzo ya hivi karibuni na baadhi ya Masista wetu ambao ni wazee zaidi kuliko mimi. Kwa kawaida, katika kuzungumza juu ya maisha yao, tunazungumza juu ya mapambano ya uhamaji, ukumbusho na upinzani. Wakati hakika kuna mashaka karibu na ukweli huu, pia nimegundua kukubalika kwa kukubalika na kuthamini kwangu mimi ni nani hivi sasa. Nimesikia Masista wakiongea juu ya kuacha haja ya kuwa na shughuli nyingi.


Niliona alama ya mambo yaliyowazunguka. Walishirikiana unyenyekevu wa sala zao, kuthamini jamii, hamu na uwezo wa kuacha majeraha ya zamani. Ninaamini kuwa ukamilifu na amani ambayo nilishuhudia katika Masista hawa ni mabadiliko kuelekea mageuzi.

Kuwa mbele ya watu ambao wanajua ubinafsi wao wa kweli, kwa sababu walichukua kazi kubwa ya kupokea mchakato wa mabadiliko, ilinipa tumaini na kunipa moyo wa kukaa katika njia hii ya mabadiliko.

Zawadi hii ya kumbukumbu ya miaka 150 ya uwepo wa ASC nchini Amerika, imetufanya tuzaliwe upya kwa kujitolea kwetu na kwa mabadiliko ya kibinafsi na ya pamoja. Kwamba tunaweza kuendelea kuwa kile ambacho Mungu anatuita kuwa.

**_Sr. Janet McCann, ASC_**

## Kama ingekuwa



Na kama ingekuwa
Kama katika vitabu vya watoto
Ambapo mbwa mwitu huongea na miti husalimia kwa kuwakaribisha;
Maua yaliyohamishwa na upepo huinama kwa furaha kusalimu
Samaki mwekundu hukonyeza kijicho na kuogelea mbali.
Je! Ikiwa jengo la shule linasema kweli,
“Habari za asubuhi”
Kwa watoto wote
Na bahari ikitabasamu, ikiita,
“Njoo ucheze nami.”
Je! Ikiwa dunia ingekuwa hai
na viumbe vyake vyote,
na haikuwa “hadithi”
Na kama ingekuwa kweli?



***Sr. Marcia Kruse, ASC***

## Kumbu kumbu ya….

Kanda ya Amerika inaadhimisha mwaka huu kumbukumbu ya miaka 150 ya kuwasili kwa Waabudu wa kwanza tisa Wajerumani huko Belle Prairie, Illinois; ilikuwa Februari 28, 1870. Tawi lingine, ishara ya uaminifu wa Mungu, lilikuwa likijiandaa kuzaa matunda. Tunaungana na Masista wa Amerika kuadhimisha tukio hili maalum.


### *Maadhimisho ya miaka 150*

Columbia Center
Jumamosi ***28 Machi 2020***

Ujumuishaji wa CPPS na sherehe ya ASC
***Jumamosi 18 Aprili 2020***

Wichita Center
Jumapili ***26 Aprili 2020***

Ruma Center
Jumapili ***12 Julai 2020***



Area Continentale: Europa
Regione Schaan




# Mkate na Mauaridi

*Nyumba ya Region ya*
*Mt. Elisabeth, Schaan/Liechtenstein*



Leo watu wengi wanatafuta mwelekeo wa kidini na Jumuiya ya kitawa.

Wengi pia huja kwenye nyumba za watawa kwa sababu hawajisikii nyumbani katika parokia hizo.

Wanatumaini huduma za kidini na sadaka kwa upande wetu ambao ni waaminifu na

hai na kwamba wanaongoza watu wazima, vijana na watoto kwa imani iliyowekwa katika maisha. Kama Jumuiya, mnamo 2003, kufuatia mwito huu, tulianza "Mkate na Mauaridi". Kwa miaka 17 sasa, kila kitu kimeungwa mkono na timu ya wasimamizi (Masista wanne wa ASC na washiriki wawili wa muda) na watu wengi wanaojitolea. Wito "Mkate na Mauaridi" – ambao unarejelea Sant'Elisabetta - kwa mfano inaelezea malengo:

**Mkate** unaashiria kila kitu tunachohitaji kila siku kuishi.

**Mauaridi** ni upendo, uzuri, heshima, Roho Mtakatifu.

**Jumuiya** ndiyo mahali ambapo mtu anaitwa kutoa na kupokea. Kwa pamoja sisi ni mkate na Mauaridi.

*Wasiwasi wetu ni kuishi na kusambaza furaha ya Imani ambayo inathibitisha uhai. Ni muhimu pia kwetu kuwaruhusu watu waliohusika kuwa na sauti na kushiriki katika malezi ya Jumuiya.*

*Mradi wa "Mkate na Mauaridi" vinakusudia kudumisha na kukuza utofauti wa Kitawa katika nchi ya Liechtenstein.Vinalenga kwa makini huduma za kiteknolojia, juu ya maandalizi ya nje ya Ushirika wa Kwanza na Uthibitisho, juu ya matoleo ya kiroho kwa watoto na vijana, na pia kwenye mikutano, semina za wikendi na mafungo kwa watu wazima. Matinee ya Jumapili asubuhi kabla ya Ekaristi ni mapokezi mazuri kwa namna ya pekee.*

***Peter Dahmen***



Regione Zagabria
Misheni ya Australia

# Habari kutoka Australia



Katika siku hizi tunamshukuru Mungu kwa mvua iliyonyesha kwenye Bara letu kavu na linalochomwa.

Hata ingawa hatukuwa katika hatari ya moja kwa moja ya moto, tunaweza kuhisi moshi ukiwasha macho yetu na koo. Wakati mwingine moshi ulikuwa sawa na ukungu ambao ulifanya mazingira ya karibu kutoonekana. Jua na anga zimebadilika rangi, kuashiria hatari iliyokaribia.

Huku Australia tupo ASC 12 ambao tumegawanyika katika Jumuiya mbili: Adelaide na Sydney. Sehemu kubwa wengi wetu tumestaafu, lakini bado tunafanya kile kinachowezekana kama sehemu ya Utume wetu. Tunawatembelea wazee, wagonjwa na watu wanaoishi peke yao, tunashirikianana watu wanaoomba msaa na ushauri wa kiroho, tunawafundisha wanaojiandaa kupokea masakramenti, tunafundisha lugha ya Kikroeshia katika shule ya Kikroeshia na tunatunza jamii ya Kroats kijamii na kiroho katika maeneo ya jangwa la Australia.

Tangu mwanzo tumekuwepo katika uhuishaji wa kiroho na mwongozo wa watu katika Nyumba ya Kardinali ya Stepinac. Nyumba ni nzuri sana na bora, watu ambao wapo, wanapokea huduma za afya pamoja na upendo wa Mungu na maridhiano kupitia neno la Mungu na maisha ya sakramenti.

Idadi kubwa ya watu wa Korintho wanaoishi huko Sydney waliijenga nyumba ya "Kardinali Stepinac", Makanisa mawili na vituo vya kusanyiko huko St Johns Park na Blacktown. Upendo kwa nchi yao ya asili umepitishwa kwa vizazi vichache, ambavyo wakati mwingine hufanya kazi katika sehemu mbili kupata pesa za kutosha na kutumia msimu wa joto huko Croatia.

Kuishi Australia ni tofauti na kuishi Ulaya. Watu nchini Australia hutumia siku nzima kazini, maeneo ya kazi ni mbali sana na nyumba zao, lakini kila kitu kimeandaliwa vizuri. Kwa sababu hii, ni vigumu sana kuwakusanya watu pamoja kuimba au kwa shughuli za burudani na hafla nyingine katika Kituo hicho. Vijana pia wana shida za lugha tangu hapo.

ufahamu wao wa lugha ya Kikroeshia ni duni sana na ili kuelewa mahubiri ya Padri, wengi wao, pamoja na familia zao, huenda kwenye parokia zinazozungumza Kiingereza.

Sydney ina idadi ya wenyeji karibu milioni 5 ya mataifa 150, uwezo wa kuishi pamoja ni mzuri sana. Kuna makanisa kutoka Jumuiya tofauti za Kikristo, lakini pia Mahekalu ya Hindu na Budha. Australia inaweza kusemwa kuwakilisha ulimwengu mdogo.

Leo Australia inafungua milango yake kwa wakimbizi na kuwasaidia kuzoea mazingira mapya haraka kama ilivyokuwa zamani na watu wa Kroatia.

Tumeitwa kuombea nchi ya Australia na watu wote, kumtia kila mtu katika Damu ya Kristo na kumtumikia Mungu kwa kila mwanadamu.

***Sr. Mara Županić, ASC***

# Sala dhidi ya usafirishaji haramu

Jumamosi tarehe 8 Februari, kumbukumbu ya Mtakatifu Josephine Bakhita mlinzi wa watumwa, huko Roma (Laterano) kwenye Kanisa la Mtakatifu Antoni wa Padua, katika mpangilio wa sala na muziki, ushuhuda na usomaji wa liturujia ulifanyika, maadhimisho ya sita kidunia ya sala na tafakari dhidi ya usafirishaji wa watu, iliandaliwa na Umoja wa Wakuu wa Italia. Jumuiya ya malezi ya kimataifa ya Waabuduo Damu ya Kristo huko Roma pamoja na Wanovisi ilishiriki pia katika adhimisho hili.

Aliyeongoza Sala hii alikuwa Kardinali Michael Czerny, katibu mdogo wa Wahamiaji na Sehemu ya Wakimbizi kwa huduma ya maendeleo ya kibinadamu.

Katika mazingira ya joto sana, ambayo yalimgusa kila mtu aliyekuwepo kwenye harakati za sala, walikuwepo pia watawa wengi kutoka Mashirika mbali mbali ya Kitawa, ambao kila siku walishiriki katika mapambano ya vita dhidi ya utumwa.

"Usafirishaji - alielezea Kardinali Czerny - unajidhihirisha katika nyanja nyingi. Labda inayojulikana zaidi ni unyonyaji wa kijinsia, lakini idadi kubwa zaidi ni ya unyonyaji mahali pa kazi. Halafu kuna hali ya kutisha ya usafirishaji wa vyombo ".


Mishumaa mitano iliwekwa altareni ikiashiria Mabara 5 na mbele ya Altare hiyo viti vitatu vitupu ambavyo viliashiria wanawake waliodhulumiwa. Matenga mengine ya matunda pia yaliwekwa kama ishara ya wafanyakazi wanaonyonywa kwenye mashamba ya nchi nyingi, kutoka Asia na Afrika, na pia alama nyingine: kitambaa cha Kiafrika, minyororo, ramani ya ulimwengu na picha ya Mtakatifu Bakhita, ambaye alikuwa muathiriwa wa utumwa.

Mkesha huo uliishia kwa kitendo cha waumini kufunga nyuzi za rangi nyingi kwa pamoja, wakiziunganisha na za jirani zao. Maadhimisho hayo yakaendelea siku iliyofuata na kuandamana kwenda Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, kwa ajili ya kushiriki Kusali Malaika wa bwana na Baba Mtakatifu Fransisco.

Kardinali Michael Czerny, akizungumza na L'Osservatore Romano, alisema: "Jibu thabiti zaidi la Kanisa dhidi ya usafirishaji haramu ulimwenguni kote, liwe la watawa. Wawe wa kwanza kuwafikia waathiriwa na kutoa msaada kadiri iwezekanavyo, kisha kuwarudisha katika jamii zao."

Maandamano kutoka kwa Castel Sant'Angelo kwenda St Peter Square yalifanyika Jumapili 9 Februari wakati wa Sala ya Malaika wa Bwana. Wakati wa hotuba yake Papa Francis alimkumbuka Mtakatifu Josephine Bakhita na kuzungumza juu ya usafirishaji haramu, akizitaka "taasisi, vyama vya Mashirika ya elimu kujitolea" kuponya "janga hili ambalo linanyanyasa wanyonge".

***Sr. Danijela Anić, ASC***



***Santa Giuseppina Bakhita***

# Kalenda ya Uongozi Mkuu

**1-7 machi:** Sr Manuela Nocco, Mhasibu Mkuu, atakutana na tume na kuangalia kwa pamoja juu ya utumiaji wa muda mrefu ya jengo la Nyumba Kuu **(imeahirisha)**
**2 marzo:** Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika atahudhuria katika Mkutano wa costellazione UISG
**3-11 marzo:** Sr. Nadia Coppa, e Sr Bridget Pulickakunnel watatembelea Foundation ya Bolivia
**4 marzo:** Ushiriki wa wanakamati katika maadhimisho ya kumbukumbu ya kuanzishwa kwa Shirika huko Acuto
**12 marzo:** Ziara ya kichungaji ya Wakubwa wetu inaanza **(imeahirisha)**
**23-28 marzo:** Sr Manuela Nocco, Mhasibu Mkuu, ataongoza Mkutano wa Tume ulioandaliwa kulingana na kitabu cha IV kinachohusu mambo ya Uchumi **(imeahirisha)**

# Sherehe za Nadhiri za kitawa

## 4 Machi 2020

### Miaka 50 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Italia

*Sr. Giuseppina Di Niro*
*Sr. Rita Scognamiglio*
*Sr. Teresa Langella*

# Siku za kuzaliwa: Tusherehekee Uhai

| | | |
|---|---|---|
| miaka 30 | | |
| **Sr Rosy Bandi** | 26/03/1990 | India |
| miaka 40 | | |
| **Sr Mary Stella Isthaky** | 09/03/1980 | India |
| miaka 50 | | |
| **Sr Matija Pavić** | 24/03/1970 | Zagabria |
| **Sr Jandira Nascimento Bar bosa** | 31/03/1970 | Manaus |
| **Sr Theresia Daniel Njau** | 31/03/1970 | Tanzania |
| miaka 60 | | |
| **Sr Alina Bilecka** | 07/03/1960 | Wrocław |
| **Sr Miriam Ortiz** | 20/03/1960 | Argentina |
| miaka 70 | | |
| **Sr Anđelka Šteko** | 02/03/1950 | Zagabria |
| miaka 80 | | |
| **Sr Dominika Santro** | 15/03/1950 | Zagabria |
| **Sr Palmina Aquilanti** | 16/03/1950 | Italia |
| **Sr Pantalea (Celestina) Morleo** | 24/03/1950 | Italia |
| **Sr Diane Tenbrink** | 27/03/1950 | USA |
| miaka 90 | | |
| **Sr Assunta Fanelli** | 01/03/1930 | Italia |
| **Sr Florence Korte** | 15/03/1930 | USA |



# Waliorudi nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 01/02/2020 | **Sr Marian Russo** | USA |
| 06/02/2020 | **Sr Elizabeth Determan** | USA |

**Gazeti la Kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*
..Kwa Neno Lako..

**Habiri ya kila mwezi**
*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA
**Mwaka XXII, N. 3, Machi 2020**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Debora Brunetti**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Johanna Rubin*** *- Kijerumani*